

TANGAZO LA SERIKALI NA. 169 la tarehe 10/03/2023

SHERIA YA PETROLI,

(SURA YA 328)

NOTISI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 50(1))

NOTISI KWA AJILI YA UGAWAJI WA MOJA KWA MOJA WA VITALU 4/1B NA 4/1C
KWA SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA YA MWAKA 2023

- | | |
|---|--|
| Jina | 1. Notisi hii itajulikana kama Notisi kwa ajili ya Ugawaji wa Moja kwa Moja wa Vitalu 4/1B na 4/1C kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania ya Mwaka 2023. |
| Mahali | 2. Vitalu 4/1B na 4/1C vilivyopo katika Bahari Kuu katika Bahari ya Hindi vinagawiwa moja kwa moja kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kama Kampuni la Taifa la Mafuta. |
| Melezo ya mahali eneo lilipo | 3. Maelezo ya eneo lililotolewa kwa mujibu wa aya ya 2 yatakuwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii. |
| Haki ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuhusiana na vitalu vilivotolewa | 4. Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania linaruhusiwa kufanya utafiti na shughuli za maendeleo katika vitalu 4/1B na 4/1C vilivyotolewa kwa kuzingatia vigezo na masharti yatakayokubaliwa kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Serikali na leseni itatolewa kwa mujibu wa sheria. |
| Kufutwa kwa TS. Na,184 la mwaka 2016 | 5. Notisi kwa ajili ya Uhifadhi wa Vitalu 4/1B na 4/1C kwa ajili ya Kapuni la Mafuta la Taifa ya Mwaka 2016 inafutwa. |

JEDWALI


(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)

MAELEZO YA KITALU 4/1B ENEO LA UCHUNGUZI

Eneo husika inajumla ya kilometa za mraba 3586.9106 kwa mujibu wa ramani ya Shirika la
Maendeleo ya Petroli Tanzania

Pointi	Latitudi	Longitudo	Lilipo
A	09° 30' 0.00" S	41° 10' 00" E	a
B	09° 30' 0.00" S	41° 40' 00" E	
C	10° 5' 29.092" S	41° 39'55.349" E	Mpaka wa Tanzania-Msumbiji
D	10° 5' 29.001" S	41° 10' 00" E	Mpaka wa Tanzania-Msumbiji

RAMANI YA KITALU 4/1B ENEO LA UCHUNGUZI




MAELEZO YA KITALU 4/1B ENEO LA UCHUNGUZI

Eneo husika inajumla ya kilometa za mraba 4538.9882 kwa mujibu wa ramani ya Shirika la
Maendeleo ya Petroli Tanzania

Pointi	Latitudi	Longitudo	Lilipo
E	09° 30' 0.0000" S	41° 40' 00" E	
F	09° 30' 0.0000" S	42° 20' 00" E	
G	09° 43' 28.629" S	42° 20' 0.081" E	Mpaka wa Tanzania-Comoro
H	10° 5' 22.537" S	42°13'14.310"E	Mpaka wa Tanzania, Msumbiji na Comoro
I	10° 5' 29.092" S	41° 39' 55.349" E	Mpaka wa Tanzania-Msumbiji

RAMANI YA KITALU 4/1C ENEO LA UCHUNGUZI



Dodoma,
....., 2023

JANUARY YUSUF MAKAMBA
Waziri wa Nishati